



**TAARIFA KWA UMMA**

## **TANZIA**



Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye, anasikitika kutangaza kifo cha **Prof. Aloyce Wenseslaus Mayo** (1960-2021), kilichotokea tarehe 1 Agosti 2021 katika Hospitali ya TMJ, Dar es Salaam.

Marehemu **Prof. Mayo** alikuwa Profesa katika Idara ya Uhandisi Rasilimali Maji, Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia. Alianza kazi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama Mkufunzi Msaidizi mwaka 1985. Alipanda vyeo vya kitaaluma hadi kufikia ngazi ya Profesa mnamo mwaka 2013, cheo alichokuwa nacho hadi alipofariki.

**Prof. Mayo** alikuwa msomi na mwanataaluma mbobezi aliyetafiti, kuchapisha na kushauri katika maeneo ya Uhandisi Mazingira. Prof. Mayo alitoa zaidi ya machapisho 100 katika majarida yanayoheshimika duniani. Alishiriki katika kazi mbalimbali za ushauri ndani na nje ya nchi. Aidha alikuwa mwenyekiti/mjumbe katika kamati nyingi za kitaaluma na za ushauri. **Prof. Mayo** pia alikua Mhariri Mkuu wa Jarida la Uhandisi na Teknolojia Tanzania.

Mipango ya mazishi ya Prof. Mayo inafanywa na familia ya marehemu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Roho ya Marehemu Ipumzike kwa Amani!

**Imetolewa na Ofisi ya Uhusiano kwa Umma  
2 Agosti 2021**